UVUNAJI

Vuna alizeti iliyokomaa. Dalili yake ni mabadiliko ya rangi ya kichwa cha mmea wa alizeti toka rangi ya kijani kuwa njano iliyoiva na kuelekea kahawia. Kata vichwa kisha anika juani vikauke vizuri mpaka mbegu inapodondoka bila kuipiga sana. Pigapiga, pepeta. Kama haijakauka vizuri, endelea kuanika baada ya kupigapiga.

Hifadhi katika gunia kwenye sehemu kavu (panga magunia juu ya mbao). Jiepushe na panya kwenye stoo.
Ukifuata haya maelekezo vizuri, tegemea kuvuna gunia 10 mpaka 16 katika ekari moja, na hata zaidi ya hapo kutegemea aina ya mbegu na menejimenti ya shamba husika na kiasi cha mvua na mtawanyiko wake katika msimu husika.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Faida MaLi

(Faida Market Link)
Eneo la Sekei (mtaa)
Barabara ya Afrika Mashariki
Mkabala na hospitali ya Mount Meru

S. L. P. 13869
Arusha
Tanzania

Simu: 027-2503549
Faxi: 027-2504080
Simu ya mkononi: 0744-962800

E-Mail: faida@faidamarketlink.or.tz
Website: www.faidamarketlink.or.tz

Faida MaLi
Soko la Uhakika ni Mali



Maelezo ya kilimo cha Alizeti

UTANGULIZI

Alizeti ni zao la mbegu za mafuta linalomea vizuri katika sehemu za joto na za baridi kiasi pia. Zao hili hulimwa zaidi kibiashara na mbegu zake hukamuliwa mafuta ya chakula. Mashudu yake ni lishe nzuri (protein) kwa ajili ya mifugo.

Udongo unaofaa ni wa mboji, wenye kina kirefu. Haihitaji mvua nyingi hasa wakati inakomaa, lakini inahitaji unyemvu wa kutosha wakati inakua na kutoa maua. Kama ilivyo katika zao la mahindi alizeti ina mbegu inayochukua muda mrefu (miezi 5) na ya muda mfupi (miezi 3 hivi).

KUTAYARISHA SHAMBA

Lima shamba kwa kutifua sana na kupiga haro ili kuua magugu yote angalau wiki 2—4 kabla ya kupanda. Kama udongo umechoka, ongeza samadi kwa wingi kabla ya kupiga haro.

KUPANDA MBEGU

Jitahidi kupanda mbegu bora kila wakati. Muulize Bwanashamba wako akufafanulie swala hilo. Kwa sehemu zenye mvua kidogo, sia mbegu mara tu mvua zinapoanza. Kwa sehemu zenye mvua nyingi, sia wakati mvua nyingi za kwanza zimepita. Panda mbegu mbili kila shimo. Nafasi kati ya mstari moja hadi unaofuata ni sentimeta 75 (mstari hadi mstari) kwa sentimeta 30 (shimo hadi shimo). Kina ni 2.5 cm – 5 cm. Ekari moja itahitaji kilo 2 ya mbegu chotara. Wiki moja baada ya kuotesha kagua shamba na rudishia mbegu katika mashimo pale ambapo haikuota, ili ujazo wa mimea shambani usipungue. Unaweza pia kusia mbegu kwa kutumia jembe la maksai. Panda mbegu mfulilizo kwa kila mstari wa 4. Panda mbegu moja moja umbali sawa na wa maharagwe (cm 15—20). Palizi kwenye alizeti ni muhimu kwa wakati kama ilivyo kwenye shamba la mahindi.

WADUDU NA MARADHI SHAMBANI

Wadudu/ Maradhi	Dalili Zake	Kuzuia/tiba
Sota (Cutworms)	Wanakata miche ikiwa michanga	• Panda mbegu iliyochanganywa na dawa.Nyunyuzia thiodan EC; Sevin 85% EC, kama uharibifu ni mkubwa.
Panya (pia ndege aina ya kwale na kanga)	Hufukua mbegu shambani baada ya kupanda na kuzila.	• Changanya pumba, chenga na sumu ya panya kisha sambaza ukingoni/mipakani mwa shamba • Mbegu ikinyeshewa na mvua mara baada ya kusia uharibifu huwa mdogo, kwani haifukuliwi kirahisi na wanyama au ndege waharibifu.
Funza wa majani na wadudu kadhaa wanaokula majani pamoja na inzi weupe.	Hukatakata na kutoboa, majani. Majani kujikunja. Inzi weupe hufyonza maji ndani ya mmea unaokua, na kusababisha unyafuzi na maradhi.	• Tumia decis, thiodan, actellic EC. Soma kwenye pakiti jinsi ya kutumia dawa. Dawa hizi hutumika pale ambapo uharibifu ni mkubwa shambani.
Kuoza ka shina mizizi au kichwa cha mmea wa alizeti. (Sclerotinia root stem / head rot)	Kuoza kwa mizizi, shina na kichwa.	• Tumia mbegu bora iliyochanganywa na dawa maalum.Badilisha mazao shambani, usiotshe alizeti kila mwaka kwenye shamba moja (Crop Rotation).Baada ya kuvuna, choma moto mabua na vichwa vyote, ili kuvunja ule mzunguko wa maisha ya wadudu waharibifu na vimelea vya maradhi.
Ndege wanao kula mbegu hususan njiwa mwitu, kwelea n.k.	Wanakula mbegu zote hasa wakati bado changa.Ndege waweza kusababisha hasara kubwa kufikia kushindwa kuvuna hata kidogo (Hasara ya asilimia mia moja).	• Otesha alizeti wakati mmoja kwa wingi katika eneo moja—Kijijini kwenu, ndege wapigwe vita kila mahali. • Panda mbegu inayokomaa kipindi kimoja, na inayoinama vichwa—wakati wa kukomaa. • Panda wakati unaostahili, usichelewe sana wala kuwahi sana • Linda ndege mara tu mbegu zinapozaliwa mpaka kukomaa kabisa. (mwezi 1 au zaidi kabla ya kuvuna). • Usipande alizeti karibu na pori, vichaka, msitu wanakoishi ndege kwa wingi.